

## **Bodi ya Maji ya Taifa (*National Water Board*)**

Usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji nchini unaongozwa na Sera ya Taifa ya Maji ya mwaka 2002 pamoja na Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji ya mwaka 2009. Sera inaelekeza kuwa rasilimali za maji zitasimamiwa katika ngazi zifuatazo:

- Ngazi ya Taifa,
- Ngazi ya Bonde,
- Ngazi ya Bonde dogo (*catchment/subcatchment*),
- Ngazi ya Wilaya,
- Jumuiya za watumiaji maji.

Majukumu ya kila ngazi yameainishwa kwenye sheria ambayo pia imetoa mfumo wa kitaasisi na kisheria wa usimamizi na uendelezaji endelevu wa rasilimali za maji.

### **2. Muundo wa Bodi ya Maji ya Taifa**

Kifungu Na. 20 cha Sheria ya Usimamizi wa Rasiimali za Maji kimempa Waziri mwenye dhamana ya maji jukumu la kuunda Bodi ya Maji ya Taifa (*National Water Board*) ambayo ni chombo kikuu cha kumshauri katika masuala mtambuka yanayohusu usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji.

Bodi hii inawajibika moja kwa moja kwa Waziri mwenye dhamana ya maji. Bodi ina wajumbe 10 na Mwenyekiti, wote wanateuliwa na Waziri. Mkurugenzi wa Rasilimali za Maji ni Katibu wa Bodi. Wajumbe wa Bodi wanawakilisha wadau kutoka makundi mbalimbali ambayo ni Serikali za Mitaa, Wizara zinazohusiana na maji (*Sector Ministries*), Bodi za Maji za Mabonde, Sekta Binafsi na Asasi za Kijamii. Wajumbe hao wanateuliwa kutokana na mapendekezeo ya wadau wenyewe.

### **3. Majukumu ya Bodi ya Maji ya Taifa**

Bodi ya Maji ya Taifa jukumu lake kuu ni kumshauri Waziri mwenye dhamana ya Sekta ya Maji katika masuala mtambuka yanayohusu rasilimali za maji, mipango shirikishi ya maji (*Integrated Water Resources Management*), utatuzi wa migogoro ya maji yenye sura ya kitaifa na kimataifa, na masuala ya kuhamisha maji kutoka Bonde moja kwenda Bonde jingine (*Inter-Basin Water Transfer*).

Majukumu mengine ni kama ifuatavyo:

- i. Kutathmini masuala yanayohusiana na usimamizi endelevu wa rasilimali za maji yatakayowasilishwa kwenye Bodi na Waziri mwenye dhamana ya Sekta ya Maji au Wizara yoyote inayohusiana na Sekta ya Maji na kutoa ushauri na mapendekezo yanayostahili kwa Waziri au Wizara hiyo ili kuwezesha kufikiwa kwa malengo ya sheria hii.
- ii. Kutoa ushauri kuhusiana na vipaumbele vyta uwekezaji (*priority investments*) na mfumo wa uwekezaji kwenye miradi ya rasilimali za maji, na kuratibu miradi na progaramu zinazogusa rasilimali za maji ambazo zinapata ufadhilli kutoka nje.
- iii. Kutoa ushauri kwenye masuala ya tathmini na mipango ya kisekta inayohusiana na rasilimali za maji (*Inter-Sectoral Water Resources Assessment and Planning*).
- iv. Kutoa ushauri kuhusiana na uratibu wa mipango na usimamizi wa rasilimali za maji kwenye mabonde ya maji.
- v. Kutoa ushauri kuhusiana na utatuza wa migogoro ya kisekta au kati ya bonde na bonde.
- vi. Kutoa ushauri katika masuala ya kuhamisha maji kutoka Bonde moja kwenda Bonde jingine (*Inter-Basin water transfer*).
- vii. Kutoa ushauri kuhusu masuala ya usimamizi wa maji shirikishi (*Trans-Boundary Water Resources Management*).
- viii. Kutoa mapendekezo kwa Waziri kuhusiana na hatua za kisheria katika usimamizi wa rasilimali za maji na udhibiti madhubuti wa uchafuzi wa vyanzo vyta maji.
- ix. Kuwasiliana na Mkurugenzi wa Rasilimali za Maji kuhusiana na masuala ya kiufundi.
- x. Kuandaa taarifa ya hali ya rasilimali za maji nchini kila baada ya miaka miwili.
- xi. Kutekeleza majukumu mengine ya kiushauri kulingana na jinsi Waziri atakavyoona inafaa.

#### **MAJINA YA WAJUMBE WA BODI**

1. Inj. Christopher Sayi - Mwenyekiti
2. Inj. Herbert J. Kashilillah - Makamu Mwenyekiti

3. Bw. Hamza Sadiki - Katibu
4. Mhe. Cynthia H. Ngoye - Mjumbe
5. Bibi. Esther S. Makwaia - Mjumbe
6. Bibi. Suzan J. Chekani - Mjumbe
7. Bibi. Janeth F. Bitegeko - Mjumbe
8. Inj. Seth P. Lusemwa -Mjumbe
9. Bi. Shukuru Y. Njati -Mjumbe
10. Herman W. Kiraryo -Mjumbe
11. Dkt. Inj. Cosmas Massawe-Mjumbe
12. Bw. Juma Shabani Mgoo -Mjumbe